

KUTOA PRESHA



Habari za asubuhi, rafiki. Nilikuwa tu nikizungumza na mchungaji sasa hivi. Na ni majaliwa makubwa sana kuja katika maskini sehemu hizi za kimbilio kama hapa. Unajisikia tu kama, vema, kuketi chini tu na kuzisikiliza ibada. Na—na kuna jambo fulani kuhusu mahali hapa padogo. Nilimwambia mwanangu, nikija kulizunguka hili jengo dakika chache zilizopita, ya kwamba mnaonekana tu kama... ningeninii tu—ningependa tu kuja hapa na kuketi na kusikiliza tu kwa muda kidogo, na kusikiliza yale wengine wanataka kusema. Sisi wahuhumu tunajua ya kwamba huo ni wakati mzuri sana kwetu. Kwa kawaida sikuzote sisi ndio tunaozungumza, mtu mwingine akitusikiliza. Bali tunapenda kuketi chini na kusikiliza pia.

2 Mnaye mchungaji mzuri, na maskini kwaya hii nzuri hapa, na nyimbo za Sayuni. Mahali hapa ni pa kupendeza sana na hapajanakshiwa kupita kiasi, na ninii tu—kile tu tungekiita nyumbani. Na kwa hiyo na—napenda hilo, vizuri sana. Mungu daima na awabariki nyote. Humm.

3 Nilikuwa... niliwazia moyoni mwangu, kumsikiliza maskini dada huyu hapa, muda mfupi uliopita, miaka sitini na mitano ya utumishi kwa Bwana. Nilidhani nilikuwa mzee kutosha kuondoka, bali nadhani mimi si mzee, baada ya hili. Huyu hapa mtu ambaye amekuwa akimtumikia Yeye miaka sitini na mitano. Hiyo ingekuwa ni kama, vema, nadhani ni kadiri ya miaka kumi na miwili, kumi na minne kabla sijazaliwa, alikuwa akimtumikia Yeye. Kwa hiyo, hilo ni zuri sana.

4 Nilikuwa nikizungumza kwenye ibada ya mazishi, hivi majuzi, kwa ajili ya maskini bi-kizee mmoja, ambaye yuna yapata umri wa miaka themanini na mitano, aliyeenda kukutana na Bwana. Na—naye alikuwa maskini mwanamke mzee mzuri.

5 Ninyi mliyoisoma hadithi ya maisha yangu, ile... ambapo nilimwomba yule mvulana kama angenihifadhia ile suti, mwajua, ambaye alikuwa na moja ya hizi suti za Wavulana wa Skauti. Nami daima nilitaka kuwa mwanajeshi, kwa hiyo nikamwomba kama angenihifadhia hiyo akiisha kuichakaza, naye akaahidi angenihifadhia. Ndipo nilipoenda kuichukua, alikuwa tu na soksi ndefu moja iliyosalia. Na hiyo ilikuwa... niliivaa soksi hiyo ndefu nikienda shuleni. Nayo ilikuwa...

6 Huyu alikuwa ni mama yake ambaye ndiyo kwanza aage dunia, Bibi Ford. Nao ni miongoni wa watu fukara sana. Llyod, huyo mvulana aliyenipa hiyo soksi ndefu, tumekuwa marafiki sana tangu tulipokuwa wavulana wadogo. Yeye ana umri mkubwa kidogo tu kuliko wangu. Basi nikamwambia,

“Lloyd, ungetaka mimi nichukue so—somo la mazishi kutoka wapi?”

7 Naye akasema, “Ndugu Billy,” akasema, “ninii tu...ni—ningetaka uzungumzie hili, kama ni mapenzi ya Bwana, hakikisho tu kwamba mama yangu atarudi tena.”

Nikasema, “Sawa kabisa.”

8 Kwa hiyo nikachukua somo kutoka katika Ayubu, “Mtu akifa, ataishi tena?” Nami nililichukua kutoka kwenye... naamini, Ayubu 14, nafikiri ndipo. Na jinsi Ayubu alivyoona ninii... Jinsi ambavyo uhai wa mimea, inapokufa, iliishi tena. Kwa hiyo nikachukua somo la, “Chochote kinachoyaishia mapenzi na kusudi la Mungu kina ufufuo.”

9 Basi nikiwa mmishenari, na kuuzuru ulimwengu, nimekuwa na majaliwa ya kuona miungu wengi na ninii zao... falsafa za maisha, na kile watu wanachoabudu. Basi katika hayo yote, hayo ni karibu yote yalivyo, falsafa, nje ya Ukristo. Ukristo unao ukweli.

10 Sasa, tunajua kwamba ulimwengu huu ni uumbaji. Na kabla hapajakuwapo na uumbaji, hapana budi pawe na Muumba wa uumbaji huo. Naye Muumba huyu hujidhihirisha Mwenyewe katika uumbaji. Kama hatukuwa hata na Biblia, bado tungalijua huo—huo—huo, huo ukweli, kama tu tuujuavyo. Biblia hii huuweka tu katika utaratibu.

11 Sasa, Mungu, akiumba viumbe, anajidhihirisha Mwenyewe tena katika viumbe. Na Yeye si Mungu tu wa Nyumba moja imara ya Upatanifu wa Sears na Roebuck. Yeye—Yeye—Yeye ni Mungu wa namna nyingi. Yeye hufanya vilima vikubwa, na vilima vidogo; pia Yeye hufanya majangwa, na—na hufanya maziwa; na Yeye hufanya miti midogo, na miti mikubwa; na maua meupe, na maua mekundu; na hufanya watu wadogo, na watu wakubwa; na wanawake wenye nywele nyekundu, na wanawake wenye nywele nyeusi. Na Yeye—Yeye hutufanya tofauti, maana Yeye anatutaka tuwe hivyo. Yeye ni Mungu wa namna nyingi. Na Yeye huwafanya wengine matajiri, na wengine maskini, wengine katikati. Bali tuna mahali pa kumtumikia Mungu, na hapo ni mahali Yeye ametuweka, kama tutadumu tu mahali hapo.

12 Nikasema, “Sasa, kama ukiangalia ua dogo.” Hii ilikuwa karibu Oktoba. Nikasema, “Mbegu...tumekuwa na jalidi sasa, na—nayo ikaangusha maskini hizo mbegu. Nalo ua likafa, nazo maskini mbegu hizo zikarudi ardhini. Naye Mungu anafanya ibada ya mazishi, katika mvua wa msimu huu wa kupukutika majani, matone haya makubwa mno ya machozi yanayotirika kutoka angani, yakizizika. Basi nikija kupitia Kentucky,” nikasema, “Hivi majuzi, kwenye kile kifua kikubwa cha milima, Yeye aliweka mashada yake kote ardhini, hayo majani mekundu, hudhurungi, manjano.” Mnaona?

¹³ Na Yeye anaomboleza kwa maana maskini mbegu hizo zimekufa, na Yeye amezizika chini ya ardhi. Naye anajua, hakika tu kadiri hiyo ardhi inavyorudi huku pamoja na mstari wa jua tena, kila moja ya hizo itafufuka tena. Lakini ni kawaida tu anayopitia Yeye, kuzungumza na sisi, kwamba kuna ufufuo.

¹⁴ Sasa tunaona jua. Linazaliwa asubuhi, nalo ni mtoto mchanga wakati linapozaliwa. Linapaswa kuipasha nchi joto na kuzifufua mbegu zilizo ardhini. Na hilo, yapata saa mbili, linaanza kwenda shule ya msingi. Na yapata saa nne ama tano, linatoka. Limepata elimu yake. Adhuhuri liko kwenye umri wake wa makamu. Saa nane alasiri, linaufikia umri wangu. Saa kumi na moja, lina umri wa baba yangu, na yule dada pale nyuma. Ndipo baada ya kitambo kidogo, kitu hicho adhimu kilichoiangaza dunia, kikatumikia kusudi la Mungu, kinakufa huko Magharibi. Huo ndio mwisho wake? Linazaliwa upya, linachomoza kesho yake asubuhi tena. Mnaona? Mungu, katika kila hatua!

Nilichukua yapata dakika ishirini, nikielezea tu kile hayo yote yalichokuwa.

¹⁵ Sasa, mnaona, basi. Nikasema, “Kwa nini?” Kunalo hitaji moja. Nami napenda kusema hili katika kanisa kama hili. Kunalo hitaji moja linalohitajika hapo. Haidhuru mbegu hiyo ni nzuri jinsi gani, haina budi kurutubishwa. Haina budi kurutubishwa. Na kama ikitekeleza kusudi la Mungu, imerutubishwa, kwa sababu nyuki huchukua chavua, na kadhalika.

¹⁶ Sasa tunaona, vipi kama maskini hilo yungiyungi, kama likininiiii...la kupendeza, lilifanya kazi kwa bidii mchana na usiku, likajifungua nafsi yake, naye nyuki anapitia pale na kuchukua tu asali yake, bure tu kama chochote kile. Hakusema neno kulihusu. Nalo lilifanya kazi kwa bidii lipate tu kutoa asali yake. Halafu basi mpitaji anaona uzuri wake. Nalo linajidumisha tu la kupendeza, kusudi mpitaji apate kuliona, anapenda urembo. Yule anayetaka harufu yake nzuri anainusa bure, nalo maskini yungiyungi hilo hufanya kazi kwa bidii lipate kujifanya msaada duniani, mnaona, kutoa asali, urembo, na maua ya mazishi, vyovyote linavyotumiwa, maua ya arusi, chochote kile. Linajitolea maskini nafsi yake bure. Ndipo linapokufa, linafufuka tena mwaka ujao. Mnaona? Kila kitu.

¹⁷ Vipi kama maskini ubua wa mahindi ungesema, “Samahani sana. Hakuna kitu cha kupendeza kunihusu mimi. Wala sina asali yoyote ya kutoa. Sikuwa na *hiki, kile, wala kinginecho.*”

¹⁸ Lakini basi Bwana wa wote aseme, “Naam, wala na maskini hilo yungiyungi lisingeweza kufanya fleki za mahindi.” Mnaona? Sisi sote—sisi sote tuna ju—jukumu tunalotekeleza. Tunamtumikia Mungu katika kundi tulilowekwa, nayo inarudi vivyo hivyo.

¹⁹ Sasa, mbele ya hayo yote, nikasema, “Huyu hapa maskini Mama Ford, kama nimjuavyo. Aliosha maskini uso wangu mchafu nilipokuwa mtoto mdogo, mara nyingi. Walikuwa ni maskini hohehahe. Lakini alizaliwa akiwa ni mwanamke, msichana wa kupendeza. Na kama alizaliwa mwanamke, hiyo ilikuwa ni kwa kusudi fulani, kuwa na mwenziwe, mwanamume. Naye akampata. Alikuwa ni mke mwaminifu. Aliishi na mumewe miaka sitini, ama zaidi, wala mwanamke mwaminifu kuliko huyu hakuzaliwa, nimjuaye, mama halisi. Kwa kuwa alikuwa katika hiyo ndoa, walikuwa wawe na watoto.

²⁰ “Hawa hapa watoto wake wazuri, wa kupendeza wanaoketi hapa, wa kupendeza tu kama yeye. Ninyi watoto msingetaka mama aliye bora zaidi. Ama, sivyo? Mnaona? La. Mumewe asingetaka mke bora zaidi.”

²¹ Nikasema, “Alikuwa ni maskini hohehahe, bali hakuna mtu angalikuja mlangoni pake, ama mhitaji, pasipo yeye kuwapa. Majirani, haijalishi walikuwa na shida gani, Bibi Ford, saa yoyote ya usiku, alikuwa hapo kuwasaidia, afanye chochote angaliweza, kwa kile alichokuwa nacho.”

²² Ndipo nikasema, “Zaidi ya hayo yote, nilikuwa na majaliwa wakati mmoja ya kuona mbegu hiyo ikirutubishwa na Roho Mtakatifu. Alizaliwa upya kwa Roho wa Mungu.” Nikasema, “Sasa tutampanda, katika muda kidogo, ardhini. Basi ni nani kwa akili timamu angeweza kusimama na kusema yeye hatafufuka tena?”

²³ “Kama ukisema hatafufuka tena, basi jani halikushuka chini ya mti kabla ya jalidi kuanguka, kujificha, lipate kurudi mwaka ujao pamoja na jani jipya. Kama huo ulikaa, utomvu huo ulikaa juu ya mti ule mpaka ukashikwa na jalidi na kugandamana, ingeua chembe ya uhai katika utomvu huo, nao huo mti ungekufa. Lakini akili fulani. . . Hauna yake wenyewe. Huo ni uhai wa mimea. Hauna akili. Lakini kitu fulani kinaudhibiti. Kabla hatujapata jalidi ama chochote kile, kwenye nchi hiyo, huko mbali Agosti, majani hayo yanapukutika mtini kwa sababu utomvu unaondoka kwenye huo mti na kurudi chini mizizini, chini kabisa ardhini, kuificha chembe hiyo ya uhai, kuirejesha tena mwaka ujao pamoja na matunda mengine.”

²⁴ Ni kitu gani kinachofanya hilo? Ni akili gani? Akili iyo hiyo huyatawala maisha yetu. Hiyo ni kweli. Na kabla hatujaweza kusema hakuna ufufuo kwa ajili ya maskini mtakatifu kama yule aliyelala pale, aliyemtumikia Mungu miaka sitini na mitano. . . Nilikuwa nikimwazia amelala pale katika hema hiyo ya oksijeni, nayo pumzi yake ikija tu. Jamani, yeye atafufuka tena siku moja. Hana budi tu kufufuka. Hivyo tu.

²⁵ Kabla hujaweza kusema yeye hatafufuka, ingekubidi kusema hakuna majira ya kuchipua, hakuna ufufuo wa mbegu, hakuna msimu wa kiangazi na wa kipupwe, hakuna kuchomoza

na kutua kwa jua, hakuna kitu kama Neno la Mungu. Mbona, ingekuwa ni wendawazimu kusema kitu kama hicho. Kunao ufufuo. Na hakika tu kama ulimwengu unavyoelea kote, na kuzunguka usoni pa jua hili tena, jua hilo litaninii. . . limepewa agizo na Mungu, kuchomoza pamoja na miali yake yenye joto, huo uhai wa mimea.

²⁶ Na mara tu wakati unapoelea huku, mpaka Umilele upambazuke tena, naye huyo M-w-a-n-a achomoze huko nje, jambo fulani litatukia. Maisha hayo yote yaliyorutubishwa ndani Yake yatafufuka tena. Hayana budi kufufuka tu. Hakuna njia ya njia nyingine yoyote. Mnaona Muumbaji akijidhihirisha Mwenyewe katika uumbaji Wake? Mnaona? Hivyo ndivyo Mungu anavyofanya. Nasi tungeweza kuangalia huko nje, mtu yeyote aliye—aliye na akili nusu, angeweza kuangalia na kuona ya kwamba Mungu, kwamba Ukristo umewekewa msingi juu ya ufufuo.

²⁷ Sasa, kama nikikiangusha kipande *hiki* sakafuni, sasa, kilishuka chini. Kisha nje hapa na kuchukua kitu kinachofanana nacho. Sasa, huo si ufufuo. Huko ni kubadilisha. Lakini, ufufuo, ni kukiinua kitu kiki *hiki*. Nasi tunarudi tena. Ninii tu. . . Ukipanda punje manjano ya mahindi, itazaa punje nyingine ya mahindi manjano. Mnaona? Nasi tunashuka, watu wapatikanao na mauti, tunafufuka watu wasiopatikana na mauti. Nasi tunafurahia sana hilo leo hii. Na hilo ni. . . Matumaini yetu yote ya Ukristo yamejengwa papo hapo, papo hapo, pekee.

²⁸ Kwa hiyo, kuja pamoja na kuketi katika mahali pa Mbinguni namna hii katika Kristo Yesu, ni majaliwa ya jinsi gani kwetu sote, vijana kwa wazee, tukiutazamia wakati huo ambapo Yesu atakuja.

²⁹ Sasa, nikiwa na kusanyiko kama hili, naye Roho wa Mungu hapa ndani jinsi alivyo, ningeweza kuzungumza mpaka saa tatu usiku, ama saa mbili, wakati wa kushuka huko chini kwenye kanisa la Foursquare, na bado niwe nikijisikia vizuri. Lakini hatuna budi kuachilia. Hawataki maharagwe yaungue, na kadhalika, mwajua. Kwa hiyo tunaingia tu kwa wakati mdogo wa ushirika, na kuwa hapa. Ndugu huyu mpendwa na kundi lake dogo, ambao mnasafiri hapa. Nasi tunakuja kushiriki chini ya mti wenu, kuketi chini na kufanya ushirika mdogo.

³⁰ Kwa hiyo hebu tulisome Neno kutoka katika Biblia ya Mungu, na tuchukue somo dogo tu na—na kuzungumza kwa dakika chache. Kabla hatujafanya hivyo, hebu na tuinamishe vichwa vyetu na kuzungumza na Mwandishi wa Hili, kabla hatujalikaribia Neno Lake.

Sijui sasa, huku vichwa vyetu vimeinamishwa, kama kungekuwako na haja mahali fulani katika hili jengo, ambayo

ungetaka kutaja, mbele za Mungu? Iweke moyoni mwako, na kuinua tu mikono yako, kwa muda mfupi tu. Mungu awabariki.

³¹ Baba yetu wa Mbinguni, kweli sisi ni watu waliojaliwa asubuhi ya leo, mbele ya ulimwengu huu unaobadilika. Nasi tumeushika mkono wa Mungu asiyebadilika. Nyakati huenda zikabadilika, bali Yeye ni wa Milele. Nalo Neno Lake liko moyoni mwetu. Ni Mkataa wa mawazo ye—yetu. Wao daima wanachukuliwa na kurudishwa kwenye hilo Neno. Haijalishi tunapotelea wapi, inarejea tu kwenye Neno. Ndiyo nguzo ya kufungia moyoni mwetu. Tunashukuru sana kwa ajili ya jambo hilo.

³² Ninakushukuru Wewe, Bwana, kwa ajili ya mahali hapa padogo kwenye Mtaa wa Arobaini na Nne, ambapo Injili inahubiriwa na mahali palipowekwa wakfu, nao watu wamejiweka wakfu Kwako. Nami naomba ya kwamba baraka Zako zitakuwa pamoja nao daima. Wazidishe katika maarifa ya Neno Lako na ya neema Yako, kisha uwape mambo mazuri ya maisha, pamoja na Uzima wa Milele, sisi sote tupate kuja mahali pamoja, ile Mbingu kuu, siku moja wakati Yesu atakapokuja.

³³ Tubariki, pamoja. Nawe uangalie mikono hiyo, Baba, iliyoinuliwa dakika chache zilizopita. Chini ya mkono huo kulikuwako na—na sababu ya kuinuliwa kwake. Ninaomba, Mungu, ya kwamba Wewe unayezijua siri za moyo utatujalia haja hii. Ninatoa maombi yangu pamoja na yao, juu ya madhabahu Yako leo hii. Jibu, Baba. Naomba katika Jina la Yesu.

³⁴ Yabariki haya Maneno asubuhi ya leo. “Tafakari za mioyo yetu zikubalike Kwako.” Libariki Neno Lako tunapolisoma. Na muhtasari kidogo wa muktadha, kwamba tuweze kueleza Hilo. Kuwa pamoja nasi na utusaidie. Ili kwamba, tutakapoondoka hapa, tunaweza kwenda na kusema, “Mioyo yetu iliwaka ndani yetu, kwa sababu tumezisikia nyimbo za Sayuni, ushuhuda wa moyo, nalo Neno likashuhudia kwa moyo wetu.” Katika Jina la Yesu. Amina.

³⁵ Sasa, mara nyingi, ninapenda tu kuzungumza. Nami siwezi kufanya hivyo kupita kiasi, kwa kuwa ni karibu saa sita sasa. Basi kwa hiyo tutawaulizeni, labda, kuyafungua Maandiko, kama ungetaka ku—kusoma Maandiko pamoja nasi, ama kuyaandika chini.

³⁶ Kwanza, ninataka kusoma kutoka kwenye Kitabu cha Methali. Ninaamini ya kwamba nilikifungua hicho asubuhi ya leo, nilipokuwa nikitafuta kote. Methali, mlango wa 18 na kifungu cha 10.

*Jina la BWANA ni ngome imara: mwenye haki
huikimbilia akawa salama.*

³⁷ Halafu basi katika Isaya 32:2, ninataka kusoma hili, 32:1 na 2.

Tazama, mfalme atamiliki kwa haki, na mkuu atatawala kwa hukumu.

Na mwanadamu atakuwa kama mahali pa kujificha na upepo, na mahali pa kujisitiri na dharuba; kama mito ya maji mahali pakavu, kama kivuli cha mwamba mkubwa katika nchi yenye uchovu.

38 Hili huenda likaonekana kama fungu la maneno la kipekee sana, kutoa maamuzi haya kutoka kwake, bali ninataka kuchukua somo asubuhi ya leo la: *Kutoa Presha*. Linaonekana linafaa sana katika siku hii. Basi nilikuwa macho muda ukiwa umeenda sana jana usiku, na—na yapata, kwenye, kati ya saa sita na saa saba, nilikuwa—nilikuwa nikijaribu kuwazia, “Sasa, niende wapi asubuhi?”

39 Nao wakaniambia, “Juu kwenye maskini lile Church of God ulilochukulia kuwa linapendeza sana, huko juu kwenye Mtaa wa Arobaini na Nne ama Barabara Kuu, yoyote iliyo.”

40 Ndipo nikasema, “Loo, nalikumbuka hilo.” Nami nikawazia, “Nitasema nini?” Nikasema, “Vema, sasa, ninakumbuka mara ya mwisho kule, nilijisikia nyumbani kabisa, kustarehe tu.” Nami nikawazia, “Hilo lingekuwa ni somo zuri, hasa, ‘Toa presha.’ Hilo ni jambo zuri la kuzungumzia, kutoka kwenye kanisa hilo dogo, asubuhi.” Na sasa . . . Nami nikaandika muhtasari kidogo hapa, nipate kutoa maelezo kwa dakika chache.

41 Nasi tunaishi katika siku ya presha nyingi. Kila mahali, kila mtu ana fadhaa nyingi. Basi moja kwa moja wanashuka barabarani na gari liendalo kasi sana, nao hawawezi kungojea taa za kusimama, na, mnajua, na wanakukanyaga. Ninii . . . Hawaendi popote, hata kidogo, hawaendi. Wanaendesha kasi tu wawezavyo, lakini wanatimua mbio tu kuelekea Umilele, ndiyo yote nijuayo. Nao . . . Nawe inakubidi kuangalia upande *huu* na upande *ule*. Na—na—na halafu ni . . . Nikasema, “Kuna matabaka mawili tu ya watu wanaoishi kule chini, na hayo ni wenye haraka na waliokufa. Nao wasio na haraka, wanakufa haraka.” Na mimi—mimi . . . Jamani! Ni hatari kuwa salama, siku hizi, ni kuharakisha, kutimua mbio.

42 Hasira? Loo, jamani! Maskini msichana mmoja, jana, mimi. . . Ndugu Williams, nadhani, hakuwa akilion. Lakini tulikuwa tukienda kupiga kona. Tulikuwa tumeenda kumwona mwanawe, naye hakuwa nyumbani. Nasi tulikuwa tukipiga kona. Ndipo maskini msichana fulani, inatupasa kuruhusia hilo, akafanya kosa kidogo. Na, mbona, mtu yeyote anapaswa kuwa, kuwa muungwana kutosha kusema, “Ni sawa, mama. Endelea. Ni sawa.”

43 Lakini ilitokea kwamba aligeuka kushoto, akageukia mbele ya jamaa fulani, na, loo, jamani. Uso wake ulikuwa mwekundu, naye alikuwa ameshusha dirisha, naye anasema tu kila kitu. Bila shaka, maskini msichana huyo alikuwa tu akizisukuma

nywele zake na kuendelea. Yeye. . . Mnaona? Ndipo huyo mtu akasimama papo hapo barabarani, karibu alikuwa akituzuia, mnaona, apate tu kumpigia makelele huyo msichana.

44 Loo, ni wakati mbaya sana! Sivyo? Tunaenda wapi? Haraka ni ya nini? Tulikuwa tukimwendesha farasi mzee kule pembeni, tunachukua wakati wetu, tukaishi muda mrefu zaidi kidogo. Nasi ni watu wa namna ile ile. Nasi hapo, loo, kila mtu akivuta sigara, a—anatoa tu moshi kwa nguvu.

45 Huko chini Tucson, juma lililopita, niliwaona watoto wamesimama. Msichana mdogo, mtoto mrembo, alikuwa na yapata umri wa miaka kumi. Naye, maskini mashavu yake, yalikuwa yemebonyea ndani kabisa. Nazo maskini nywele zake, nyeusi, maskini jamaa aliyeonekana wa kupendeza sana. Naye alikuwa amesimama hapo, akivuta sigara kabla hajaingia. Sasa, mtoto huyo labda alikuwa na TB, labda mwenye wasiwasi tu kupindukia. Sasa, labda sababu ya yeye kuvuta sigara, mama yake alivuta sigara kabla yake.

46 Nilikuwa kwenye Maonyesho ya Ulimwengu mwaka huu, nami nadhani wengi wenu mlikuwa huko. Nami nilifurahia kitu kimoja, hicho kilikuwa ni kile Chumba cha Matibabu. Basi walipokuwa kule, wakithibitisha yale uvutaji wa sigara unayofanya, walikuwa na huyu Yul Brynner, na—nanyi mlikuwa kule, mliona hilo. Basi walichukua sigara, wakaiweka kwenye ki—kitu fulani, kisha wakavuta moshi nje, na kuutapanya kote kwenye kipande cha marmar nyeupe, kisha wakaipangusa hiyo sumu ya tumbaku kwa kipande cha pamba, na kuiweka mgongoni mwa panya. Na katika siku saba kulikuwako na kansa nyingi sana, huyo panya hata hangeweza kutembea, kutokana na sumu hiyo ya sigara moja.

47 Ndipo huyo daktari akasema, “Mmewasikia watu wakisema. . .” Ndipo akaigeuza, na kuiweka chini ya tyubu, na kuacha moshi huu usukumwe kupitia namna fulani ya kemikali, napo palikuwa na mchirizi mweupe. Akasema, “Hiyo hapo kansa.”

48 Kisha akasema, “Mmewasikia watu wakisema, ‘Mimi siivuti ndani ya mapafu.’” Kwa hiyo akaivuta kinywani mwake namna hiyo, akaivuta ndani, kisha akaweka kinywa chake kwenye tyubu hii na kuipulizia, na karibu hakukuweko na yoyote ndani yake, hata kidogo. Akasema, “Kansa iko wapi? Kinywani mwangu. Ninaimeza kupitia kooni mwangu. Linaichukua, koo langu, nayo inaingia tumboni.” Halafu basi huyo alikuwa ndiye aliye bora kuliko wote ulimwenguni, kumbukeni.

Ndipo anaendelea na kusema, “Watu husema, ‘Tumia ncha yenye chujio.’”

49 Mmesikia hilo, “Moshi wa mtu mwenye busara,” ama namna fulani ya msemu. Kama huyo mtu ana busara, hata kidogo,

hatavuta sigara, hata kidogo. A-ha. Sio mtu mwenye busara; ni mtu asiye na busara, ndiye angevuta moja.

⁵⁰ Lakini, yeye aliivuta tumbaku hii. Akasema, “Sasa, mnaona, jambo tu ni kwamba, umma si mwerevu vya kutosha kung’amua hili, na hata hivyo tunadhaniwa kuwa ni watu wenye akili.” Kasema, “Kama hupati moshi, hupati matokeo yoyote. Na unapopata moshi, huna budi kuwa na lami ili upate moshi. Nayo lami ndiko kansa ilipo. Inahitaji lami kufanya moshi.” Tena kasema, “Jambo pekee, kuzivuta zikiwa na ncha, unavuta kama tatu, kupata ridhaa ya moja huo wakati mwingine. Unapata kiasi kile ndani yako, hasa.” Unaona? Nao umma wa Marekani wanapenda kufanyiwa mazingaombwe. Wanayo. Hiyo ni kweli. Haya basi. Mnaona?

⁵¹ Ndipo walipomtoa huyo panya nje. Walikuwa wamemtoa mmoja nje, kila siku saba. Ilikuwa ndiyo tamasha ya kuchukiza sana niliyopata kuona. Kulikuwako na jamaa mkubwa mnene aliyeketi karibu nami, kasema, “Whiu,” jasho likitiririka kutoka kwake. Akasema, “Ajabu sana!”

Nikasema, “Je, wewe huvuta sigara?”

Akasema, “Naam.”

⁵² Haya basi, lakini hata hivyo, tunaendelea moja kwa moja kuvuta. Kwa nini? Tunajaribu kupata kitu cha kutuliza, nusukaputi fulani. Inaonekana kana kwamba ulimwengu umo katika mwendo wa hatari sana, nami sijui kile—kile wanachomaanisha.

⁵³ Bali kuna nusukaputi ya Kikristo. Kuna a—afyuni, inayotoka kwenye yungiyungi. Nalo kanisa la Kikristo lina afyuni, na imetoka katika Yungiyungi la Bondeni. A-ha. Hutuliza maumivu yote. Nao umekwisha kabisa basi, unapopata afyuni hii ya Kikristo. Divai hii mpya waliyokuwa nayo kwenye Siku ya Pentekoste, mnaona, hutuliza maumivu.

⁵⁴ Watu, wana kiburi sana, nao wanafanya mambo wasiyopaswa kufanya. Badala ya kujaribu kuondoa chanzo chake, wanaiongezea tu chanzo kingine. Kamwe huwezi kupata tiba mpaka uondoe chanzo chake.

⁵⁵ Mwanadamu anajaribu kutafuta kitu cha kuridhisha, naye anaona kiu. Na Mungu alimfanya kuona kiu. Ambapo, yeye aliumbwa hivyo, bali Mungu alimwumba hivyo apate kumwonea Yeye kiu. Bali yeye hujaribu kuiridhisha, na kuutuliza wito huo mtakatifu ndani yake, kwa mambo ya ulimwengu. Nasi hatuna haki ya kufanya jambo hilo. Sasa, lakini watu hufanya kosa, sikuzote. Badala ya kwenda mahali pale kuondoa chanzo chake, sisi hujaribu kukituliza kwa nusukaputi, na pombe, na kuvuta sigara, na kuweka mengi zaidi kwake, kukilundika, wakati wote, tukikifanya kibaya zaidi. Na yote haya yanapandisha tu presha. Inakifanya tu kuwa kibaya zaidi, wakati wote. Sio muda mrefu uliopita . . .

⁵⁶ Ninyi, nyote—nyinyi nyote labda mnajua ninalenga shabaha sana na kuwinda. Hayo ndiyo niliyo nayo kama kiburudisho. Ndugu fulani alikuwa ameagizia kwa—kwa Kampuni ya Weatherby na kuchukua Winchester mu—muundo 70, kama baadhi ya wawindaji wenzangu humu ndani wangejua. Nayo ilikuwa imepanuliwa shimo ikawa Weatherby chapa .257. Art Wilson alimpa Billy Paul bunduki hiyo, naye hutumia mkono wa kushoto. Nayo ilikuwa na komeo, ndipo akanipa tu.

⁵⁷ Jamaa mwingine akaingia, kasema, “Wewe huna Weatherby, kwa hiyo nitakupanulia shimo.”

⁵⁸ Basi katika kulipanua hilo shimo, hawakutaka kukubali, bali hawakulipanua vizuri. Basi walichofanya, kurudi. . . Ninyi mnaotia kwa mkono mnafahamu, kwamba, nyuma ya duara ilikuwa ikipata joto. Ndipo niliporusha mfululizo mchache wa risasi ndani yake, niliona baruti ilikuwa ikirudi nyuma, na kulikuwa na presha. Vema, nilijua risasi hiyo ilikuwa imetiwa chini ya uzito wa juu zaidi, kwa hiyo isingeweza kuwa inapata presha kutoka kwa hiyo. Lakini haikuwa imepanuliwa shimo vizuri.

⁵⁹ Basi ile risasi nyingine iliyowekwa, kama haikuwa ni Mungu, ningaliyapoteza maisha yangu. Ilininii tu, bunduki yote, ililipuka na kuilipukia miti iliyonizunguka, namna hiyo. Urefu kama wa jengo hili, moto mwekundu ulilipuka. Ndipo mtutu wa bunduki ukarushwa kwenye huo uwanja wa shabaha wa yadi hamsini, nalo komeo likapitia juu ya kichwa changu, namna *hii*. Darubini ikalipuka, karibu *hivi* na macho yangu. Na—nami sikuwa na chochote mkononi mwangu; ililipuka tu.

⁶⁰ Damu ikibubujika kwa kila njia, kutoka karibu nami, nasi tulikuwa mbali sana na daktari. Nao wakaniona. Nami nisingeweza kuzungumza wala chochote kile. Nami nilikuwa nikizuilia damu yangu ndani, namna *hii*. Nikaiondoa, nayo ikambubujikia kote ndugu aliyekuwa amesimama pale, nami nikairudisha.

⁶¹ Nikasema, “Bwana Yesu,” moyoni mwangu, “Wewe ndiye Mponya wangu.” Nikaushusha mkono wangu. Ikakoma.

⁶² Kwa hiyo shida ilikuwa ni nini? Hiyo bunduki ilikuwa ikijaribu kurusha risasi ambayo kweli haikutengenezewa hiyo bunduki. Kama bunduki hiyo ingalikuwa imeundwa tangu mwanzo, Chapa ya Weatherby, isingalilipuka. Bali ilikuwa ni kujaribu kuweka risasi ya Weatherby katika bunduki ya Winchester, na haingefanya kazi.

Nanyi mnaona makovu huku *kote* na juu ya macho yangu, na vipande kumi na vitano vilienda chini kidogo tu ya jicho. Daktari alipoliangalia jicho langu, alimwandikia tena rafiki yangu, daktari. Akasema, “Jambo pekee nilijualo, ni kwamba Mungu alikuwa ameketi kwenye hiyo benchi pamoja na mtumishi Wake. Mtu huyo alikuwa pamoja naye, huko nje kwenye. . . akiongoza,

angepatikana tu kuanzia kiunoni kwenda chini.” Kasema, “Mungu alikuwa pamoja naye.” Kisha kasema, “Risasi hiyo, vi—vile vipande vya baruti, viliweka vipande kumi na vitano moja kwa moja nyuma ya mboni ya jicho, chini tu ya jicho.” Haikunisumbua hata kidogo. Siku mbili ama tatu baadaye, uso ulionekana kama hambaga, wote ulikuwa umekauka ukaisha.

⁶³ Lakini ilikuwa ni kitu gani? Ilikuwa ni kwa sababu ilikuwa ni risasi katika bunduki ambayo si yake. Ilikuwa imepandisha presha. Sasa, kama bunduki hiyo ilikuwa imetengenezwa, na katika kishikizo hiki ambapo risasi iliingiziwa kutoka kwenye chemba kuingia kwenye mtutu, hiyo chemba, kama chemba hiyo ilikuwa imefanywa vizuri, ingalistahimili hiyo presha. Nayo presha inatokea hivi. Lakini badala yake, ilikuwa imelegea. Nayo presha hiyo, ile risasi ikiwa ni dhaifu kuliko mtutu, bila shaka, ililipukia upande *huu*, na kuilipua bunduki nyuma *hivi*.

⁶⁴ Mtutu haukudhurika; iliuraria tu. Bila shaka, ilirarua kabisa kila kitu karibu nayo. Isingeweza kutumika tena. Lakini kifuniko kilikuwa kingali kimetokeza katika mtutu. Mnaona, haikuwa... Sasa, kama ingalikuwa ni risasi iliyoshindiliwa kupita kiasi, ingaliulipua huo mtutu. Lakini, mnaona, hapa ndani, sehemu iliyo nene sana ya bunduki, ililipukia nyuma *hivi* na kuilegeza kufuli. Sasa, kama ilikuwa imetengenezwa, chapa ya Weatherby, kamwe isingalilipuka. Ilikuwa ni kujaribu kuweka kitu katika kitu ambacho hakikuwa cha mahali hapo.

⁶⁵ Hiyo ndiyo njia ya ujuzi wa Mkristo, wakati watu wanapojaribu kuweka maungamo baridi, ya kawaida katika Kanisa lenye nguvu la kipentekoste, ama ujuzi, isipokuwa mtu huyo amejengwa kutoka chini kwenda juu, amejengwa kabisa, akazaliwa mara ya pili, akafanywa upya. Waigaji wa siku hizi, wanazunguka, wakijaribu kuiga kunena kwa lugha, wakijaribu kuiga *hiki* na kuiga *kile*, zile karama, kama hawajazaliwa mara ya pili.

⁶⁶ Na iwapo wamezaliwa mara ya pili, hawawezi kuiga, kwa sababu walijengwa kwa ajili ya mambo hayo. Wamezaliwa, wakafanywa upya, wakafinyangwa tena; sio kitu tu ambacho kimebandikwa, na kupewa mikono, na kupata muhemko, na kucheza kuyazunguka madhabahu mara chache, na kusema, “Ninayo.” Ni kitu ambacho kimefinyangwa tena, na kufanywa upya, kikawa kiumbe kipya. Ndipo kinaweza kustahimili presha ya mateso na mambo yanayoyafuata maisha ya kiroho. Huna budi kufanywa na kujengwa kuistahimili presha. Na kuna jambo moja tu linaloweza kufanya hilo. Hilo ni wakati unapoingia kwenye nyumba ya Mungu ya kufinyangia, na kuvunjiliwa mbali na kujengwa upya, kiumbe kipya katika Kristo Yesu.

⁶⁷ Nilikuwa hapa nje nikienda hapa hospitalini, sio muda mrefu uliopita, na mimi—mimi nilikuwa nikienda kumwomba mama fulani. Na palikuwapo na mama mwingine aliyelala

karibu naye. Nami nikamwona ana wasiwasi sana, nami nilikuwa ninaanza kuzungumza juu ya maombi. Ndipo nikasema, “Vema, tutaviinamisha vichwa vyetu kwa ajili ya maombi,” nikasema.

⁶⁸ Akasema, “Ngoja kidogo! Ngoja kidogo! Ngoja kidogo! Shusha hilo pazia.”

Nikasema, “Naam, mama.” Nikasema, “Nilikuwa tu nikitaka kuomba.”

Naye akasema, “Vuta pazia hilo.”

Nikasema, “Naam, mama. Hivi wewe si mwaminio?”

Naye akasema, “Sisi ni Wamethodisti.”

⁶⁹ Nikasema, “Vema, hilo bila shaka linaelezea yale niliyouliza.” Mnaona? Naam. Naam. Naam. Mnaona? Naam. Kamwe sikumwuliza alikuwa ni wa chama gani. Nilimwuliza kama alikuwa ni mwaminio. Mnaona?

⁷⁰ Vyama hivi vyote hutuchanganyisha kabisa. Huwezi kujiunga na kanisa. Hakuna kitu kama hicho. Unaweza ukajiunga na chama. Unaweza kujiunga na chama cha Kimethodisti, chama cha Kibaptisti, chama cha Kipresbiteri, ama chama cha Kipentekoste. Bali huwezi kujiunga na Kanisa. Huna budi kuzaliwa. Hiyo ndiyo sababu, tuna milipuko mingi sana. Mnaona? Presha inapanda, nawe huyo unalipuka. Unasema, “Vema, mimi ni mfuasi wa *hili*.” Lakini hilo halimaanishi...

⁷¹ Inakubidi kuja kutoka chini, kwenda juu, upate kuistahimili presha ya siku hizi. Wakati Mungu anapoweka chaji Yake kuu ya Roho Mtakatifu mle ndani, afadhali ujue yale unayofanya. Afadhali ujiandae kwa ajili yake.

⁷² Sasa, kama wewe—kama kwa namna fulani umetoboa upya kitu fulani, useme, “Nilikesha usiku kucha kwa ajili ya karama,” afadhali uwe mwangalifu. Huenda ikalipuka, unaona, nayo itaenda kinyume na matarajio.

⁷³ Nikija hospitalini, niliwazia, nilikuwa nikishuka usiku mmoja, ndipo—ndipo nikatumiwa... Ilikuwa ni Ndugu Neville, simu ya mchungaji, na mimi—mimi—mimi nikaichukua, maana nilikuwa nikitoka Louisville. Nayo ilisema mama huyo alikuwa mahututi sana. Basi nikaenda hospitalini kule Jeffersonville, na kulikuwako na mama pale. Na mimi... Waliniambia, “Nenda kwenye chumba 322. Huyo mama alikuwa kule.”

⁷⁴ Nikaingia ndani. Nikasema, “Je, kunayo wadi ya vitanda ‘vinne’?” Nikasema, “Kuna mama, *Fulani-wa-fulani*, hapa?”

“La, bwana. Hayupo hapa.”

Nikasema, “Labda nilikosea. Samahani.”

⁷⁵ Ndipo nikarudi nikatoka. Naye nesi alikuwa akishuka sebuleni, na kidogo alikuwa na haraka. Nikasema, “Mama,

waweza kuniambia kama mama fulani yuko hapa juu kwenye wadi hii, ama mahali alipo?”

⁷⁶ Akasema, “Sina wakati wa kufanya mambo kama hayo. Na kwani wewe huwezi kuona nina haraka?”

Nikasema, “Samahani.”

⁷⁷ Nikaenda kwenye dawati, na—naye huyo mama alikuwa ameketi pale kwenye dawati, nesi. Basi nikasema... Alikuwa akiandika kitu fulani. Nikaendelea kungojea. Akaniangalia; akaendelea tu kuandika. Vema, nikangojea hapo dakika chache. Nikasema, “Habari za jioni.” Kamwe hakusema kitu. Ndipo nikawaza, “Vema?” Nikasema, “Waweza kuniambia mahali mama fulani alipo? Ni... Mimi ni mhudumu. Nimetumwa hapa mahali fulani, kwenye chumba 322, waliniambia.”

Naye akasema, “Vema, basi nenda kwenye chumba 322.”

Nami nikasema, “Mama, nimekuwa kwenye chumba mia tatu-...”

Akasema, “Kwa nini kuniuliza, basi? Nenda kwenye dawati la orofa ya chini.”

Nikasema, “Vema, asante.”

⁷⁸ Nikaanza kushuka kwenye orofa ya chini, ndipo nikafika kule. Nami nikamwuliza nesi aliyekuwa hapo chini. Hakujua lolote kulihusu.

⁷⁹ Huyu hapa maskini daktari mmoja anakuja, akipitia kwenye orofa hiyo, pamoja na stirioskopu zake mkononi mwake, akizizungusha-zungusha, namna *hii*. Maskini... Sijawahi kuona mtu mnene jinsi hiyo! Yeye alikuwa—yeye alikuwa... Kwa kweli, ninaamini alikuwa mpana zaidi ya alivyokuwa mrefu. Alikuwa akitembea... ama, “yeye alikuwa juu, hasa.” Kwa hiyo alikuwa akishuka, akizizungusha hizi stirioskopu mikononi mwake. Nami nikasema, “Samahani, daktari. Unaweza kuniambia mahali...”

Akasema, “Naam, naam, ni huko nyuma, *huko*,” akasema.

“Asante, bwana.”

⁸⁰ Nikashuka chini upande huo mwingine. Nikawaza, “Vema, sasa, nitafanya nini?”

⁸¹ Ndipo akashuka chini, akaketi nyuma ya dawati. Nami sikumwona mtu mwingine. Nikafikiri afadhali nitembee huko juu na kumwuliza tena. Nikasema, “Samahani, bwana.” Akaendelea tu kuangalia kitu kingine, mwajua. Nami nikasema, “Hivi... Ninataka kujua mahali chumba...”

Kasema, “Ni nyuma upande *ule*.”

Nikasema, “Chumba 222, siwezi kujua jinsi ya kwenda.”

Akasema, “Nenda tu *hivi*, na *vile*. Utakipata.”

⁸² Ni kitu gani? Presha, mnaona, presha inapanda. Huenda alikuwa ametoka kwenye upasuaji. Huenda alifikiria ya kwamba alikuwa...kwamba sipaswi kuwa nikimwuliza hilo. Ilikuwa imepita saa za kutembelea, kweli. Kisha akawazia, “Mhubiri fulani tu. Acha aende.” Mnaona?

⁸³ Ulimwengu umejengwa tu juu ya presha. Utalipuka, moja ya siku hizi. Ulimwengu, umejaa presha, nao madaktari hawajui la kufanya juu yake. Wataalamu wa akili wana wataalamu wa akili wakiwatibu. Hiyo ni kweli. Hawana jibu, bali Mungu analo. Mungu analo jibu kwa haya yote.

⁸⁴ Katika Agano la Kale, wakati mtu alipokuwa amefanya kosa, sasa, ilikuwa ni jino kwa jino, na jicho kwa jicho. Na kama mtu huyu alifanya kosa fulani, alikuwa na mahali pa kukimbilia. Ninaamini Yoshua alikuwa amejenga nyumba za kukimbilia. Basi kama watu walikosea, nao walistahili kuuawa, lakini walikuwa na mahali pa kimbilio ambapo mtu angeweza kukimbilia, mji huu wa kimbilio. Naye alikuwa salama kama waliomfukuza hawakumshika kabla hajafika kule. Yeye... Lakini kama wenye kumfukuza walimshika, wa—walimwua, njiani.

⁸⁵ Lakini kama alifika kule, na kama alikuwa ametenda uhalifu huu pasipo kukusudia na angeweza kujitetea, na kuonyesha ya kwamba a—alikuwa amejutia kitendo hicho, basi angeweza kuletwa kwenye mji huu wa kimbilio, nao waliomfuata wasingeweza kuingia kwenye mji huu. La. A—alikuwa salama. Hiyo ilikuwa ni hisia ya namna gani, kujua ya kwamba ulifanya jambo—jambo baya, nawe unajua lilikuwa baya, bali kuna mahali ambapo haitakubidi kufadhaika tena, unaingia mahali hapa na unakuwa salama.

⁸⁶ Sasa, kama huyo mtu alifanya hivyo makusudi, vema, basi ilimbidi ku...Yeye, asingeweza kuingia. Kama alikuwa amefanya mauaji makusudi, kesi yake ilifanyiwa langoni. Na hiyo ni...Lakini mtu aliyetaka, wala hakufanya hivyo makusudi...

⁸⁷ Kama tu vile ningetoa mfano wake. Kama mtu amefanya kosa, naye kweli anataka...yeye, yeye anasikitika kwamba alitenda dhambi, kuna mahali pa kimbilio. Lakini kama yeye hajali tu, basi hakuna mahali kwa ajili yake, maana hatalikubali. Tayari amefanya ukatili, naye alitaka kufanya hivyo, hakuna nafasi kwao. Na hivyo ni kama ilivyo leo hii.

⁸⁸ Halafu basi, jambo lilikuwa, kama alikuwa amekosea sharti atake mahali pa kimbilio. Lazima atake kuwa huko.

⁸⁹ Na huo ni mfano mzuri sana wa kanisa siku hizi na watu. Mtu lazima atake mahali pa kimbilio. Huna budi kujisikia ya kwamba unapahitaji. Lakini kama unajisikia unataka kupiga vita vyako mwenyewe, endelea. Mnaona? Lakini una hakika

kushikwa na wanaokufuata. Lakini siku moja itakupata. Bali kama unataka mahali. . .

⁹⁰ Halafu wakati mtu huyo anapotaka mahali, na amepata mahali, hana budi kuwa radhi kukaa hapo. Hutoki nje tena. Unakaa hapo, ndipo uko salama wakati ukiwa hapo. Loo, ilikuwa ni faraja jinsi gani, kupata mahali. Mara unapoingia malangoni, nayo malango yakafungwa nyuma yako, ningeridhika. Naam, bwana.

⁹¹ Hana budi kuwa radhi kukaa hapo, pasipo kunung'unika; kutembea huku na huku na kusema, "Loo, ni kwa nini hata nikaja hapa?"

⁹² Sasa, hivyo ndivyo tu watu wanavyofanya siku hizi. Wanasema wanataka kuwa huru na masumbuko ya ulimwengu, halafu wanaingia katika. . . miongoni mwa waaminio, halafu basi wanasema, "Sasa, kama itanibidi kuachana na *hili*, kama itanibidi kufanya *vile*, kama itanilazimu kutoa zaka, kama itanibidi kufanya *haya*, na mambo *haya* mengine, jinsi, loo, jamani! Kitu gani?" Mnaona? Basi mtu huyo, akinung'unika, alirudishwa tena, ukajitegemee. Lakini kama angeninii. . . Hana budi kuridhika, na asilalamike.

⁹³ Loo, jinsi ninavyopenda kusema jambo hili! Kamwe sijataka kutoka nje tena. Loo, ni Mbinguni, kwangu mimi, kuketi katika mahali pa Mbinguni katika Kristo Yesu, pamoja na wanaume na wanawake waliokimbilia maisha yao, kutoka kwa mambo ya ulimwengu, na kutia nanga nafsi yao katika mahali pa raha. Loo, ni ushirika wa jinsi gani! Loo, ni furaha ya Kiungu ya jinsi gani! Kuegemea kwenye Mkono Wake wa milele, presha yote imekwisha. Pasipo kuhofia chochote, amina, kwa kuwa mimi ni salama katika Kristo.

⁹⁴ "Yeye ni Ngome imara, wenye haki humkimbilia Yeye wakawa salama. Yeye ni Mwamba katika nchi yenye uchovu, Kimbilio katika wakati wa dhoruba." Ni mahali pa jinsi gani kuwa! Si—sioni kitu cha kulalamikia. Lalamiko pekee nililo nalo, kwa nini sikufanya hivyo muda mrefu kabla sijafanya? Nilingoja mpaka nikawa na yapata umri wa miaka kumi na tisa, ishirini. Inanipasa ku. . .

⁹⁵ Jamaa fulani alikutana nami hivi majuzi, jamaa mdogo. Nami nilikuwa nikizungumza kuhusu hii, kashfa hizi za wanawake hawa huku nje mtaani, waliovaa mavazi haya, wakionekana kama wanaume. Nami nilikuwa nikilikemea vikali sana. Jamaa mdogo akakutana nami nje ya mlango. Akasema, "Hebu kidogo."

⁹⁶ Na kufanya vurumai hii hapa, mwajua, kujinengua, wakivunja miguu yao, na kila kitu. Nikasema, "Ni wendawazimu." Kisha nikasema, "Mkristo halisi, kama hilo liko moyoni mwao, nao wanadai kuwa Mkristo, ma—matunda yao yanaonyesha kile walicho." Inaonyesha utupu,

kwa mwanamume ama mwanamke yeyote kujaribu kujiridhisha juu ya upuuzi wa—wa ulimwengu, machukizo ya ulimwengu; wakijaribu kujiridhisha, wakati Sayuni imejaa uzuri na nguvu. Kuridhisha, kutoa presha, kwa nini ubadilishe chakula cha Malaika kwa vitunguu saumu vya Misri, kama vile Israeli walivyotaka? Loo, kuna mahali pa kutolea presha! Ingia mle, nawe utakuwa salama utakapoingia mle. Ni kitu cha ajabu jinsi gani kujua hilo! Vema. Hakuna kulalamika.

⁹⁷ Huyu kijana mwanamume aliniambia, akasema, “Angalia, Bw. Branham.” Kasema, “Wewe ni mtu, umri wa miaka hamsini.” Kasema, “Wewe hutamani urembo wa wanawake unapowaona wakitembea.” Nikasema... Kasema, “Kama ungalikuwa wa umri wangu...” Alikuwa na kama ishirini na mitano. Akasema, “Kama ungalikuwa wa umri wangu, ungeona tofauti.”

⁹⁸ Nikasema, “Bwana, nilikuwa nikihubiri Injili ii hii, mdogo wa umri kwa miaka kadhaa kuliko ulivyo sasa. Nilipata tu kitu kilichoridhisha, kitu kilicho halisi, kitu fulani, hata vingine vyote ni vipofu.”

⁹⁹ Niko ndani ya Ngome. Hata sina tamaa ya kuangalia nje. “Yeye anayeshika plau, na hata ageuke kuangalia nyuma, hastahili kulima na plau.” Ni mahali pa jinsi gani kuja! Naam. Huko nje unakufa; ndani uko salama. Ingia tu na kutoa presha. Hilo ndilo jambo la kufanya. Naye Kristo ndiye Ngome yetu, naam, mahali palipowekwa na Mungu pa usalama. Yoshua alijenga hizo nyumba na hiyo miji ya kimbilio, naye Mungu alitujengea mji wa kimbilio, huo ni katika Mwana Wake, Kristo Yesu. “Jina la Bwana ni Ngome imara. Wenye haki huikimbilia wakawa salama.”

Sasa mnasema, “Vipi kama ukiwa mgonjwa humo ndani?”

¹⁰⁰ Yeye alichukua maradhi yetu, katika Ngome hii tuliyo ndani yake. Yeye alichukua maradhi yetu, mwilini Mwake. Tuna ninii...

¹⁰¹ “Vema,” mnasema, “vipi kama ukichoka wakati ukiwa humo ndani, masumbuko yote na kadhalika?”

¹⁰² Mtwikenii fadhaa zenu. Imeandikwa kwenye kila ukuta, kote kote, kila mlango. “Mtwikenii fadhaa zenu, kwa sababu Yeye anawajali.”

¹⁰³ Litumainie Neno Lake lililoahidiwa. Maneno Yake yameandikwa juu ya moyo wetu. Mioyo yetu ndiyo meza za Neno Lake, kama vile Martha na Mariamu, na kote kote. Mnaona?

¹⁰⁴ Hata mauti yenyewe hayakufadhaishi hapa ndani, wakati ukiwa katika Bwana. Kwa nini? Yeye alifufuka katika wafu. Hatuna wasiwasi wowote juu ya hilo. Mauti huja, kama maskini dada yule tuliye kuwa tukizungumza juu yake pale. Ikiwa ni

wakati wa kwenda, haya twendeni. Hiyo ni kweli. Unafanya nini? “Unabadilisha maskini mzoga huu wa kuchukiza tulio nao, kwa mwili usiopatikana na mauti uliofanywa kama mwili Wake mwenyewe uliotukuka.” Ni nani asiyeweza kuibadilisha nyumba hii ya wadudu kwa kitu kama hicho? Niambiieni mtu fulani ambaye asingeibadilisha. Mzee, kijana, haijalishi kama una umri wa miaka kumi na mitano tu, ama kumi na miwili, ama wowote ule, mauti yamekaa mlangoni pako. Hujui ni wakati gani. Moyo huo wa binadamu unaodunda namna *hii*, hauna budi kusimama, siku moja. Nao huenda ukasimama wakati ukiwa na umri wa miaka kumi, kumi na miwili. Husimama, kwa maelfu, kila siku. Lakini hapa ndani, katika . . . Mwili huu ambao tutaubadilishia, damu haiupigi huo. Roho Mtakatifu huupiga. Wala hauwezi kufa. Haupatikani na mauti, wa Milele, na hauwezi kufa. Ni ahadi ya jinsi gani! Naam, hata mauti, hukoma.

¹⁰⁵ Waangaliieni Israeli. Sasa, kulikuwa kunakuja mvua ya mauti kote Misri, naye Mungu akafanya maandalizi. Yeye aliwafanyia kimbilio. Ndipo Yeye akasema, “Chukua mwana-kondoo ukamchinje, kisha uweke hiyo damu kwenye miimo na mlangoni. Ndipo nitakapoiona hiyo damu, nitapita juu yenu.” Misri ililicheka hilo, bali ilikuwa ni njia iliyowekwa na Mungu ya kuwakinga na mauti. Na sasa, wakati hayo mabawa makubwa meusi ya mauti yalipoenea kote m—mji, na mji baada ya mji, kote Misri, nayo hayo mauti yakaanza kuingia katika kila nyumba, na vilio vikitokea; ninaweza kuwaona Israeli, wametulia tu, wakatoa presha.

¹⁰⁶ Mvulana mdogo huenda alimwendea baba yake, na kusema, “Baba, unajua, ndio kwanza nimsikie yule mkimbiaji akipita mtaani. Mtoto Johnny niliyecheza naye kule chini, amekufa. Na, baba, mimi ndiye mzaliwa wako wa kwanza.”

¹⁰⁷ Namwona maskini baba huyo akisimama, anatoa miwani yake, tuseme, anaiweka Biblia yake chini, anasema, “Njoo hapa, mwanangu.”

“Baba, anashuka kuja mtaani.”

“Toa presha, mwanangu. Njoo hapa kidogo. Unaona ile damu?”

“Naam, ninaiona, baba.”

“Vema, toa presha.”

¹⁰⁸ Kadogo, haikubidi kukimbia mtaani kwa gari lako liendalo mbio sana. Haikubidi kufanya mambo haya. Chunguza tu uone kama damu iko pale. Toa presha. Iwapo mauti yanapiga hodi mlangoni, hayawezi kufanya lolote.

¹⁰⁹ Hakuna presha kwa Israeli. Wangeweza kutoa presha, kwa sababu walikuwa salama chini ya damu. Loo, jamani! Huo usiku mkuu wa pasaka, hapana shaka walikuwa watulivu, wametoa presha, maana wangeweza kuchunguza na kuona walikuwa

na ile damu. Basi walipoiona ile damu, walijua Yeye aliahidi angepita juu. Loo, baada ya wao kufuata maagizo yote ya Mungu, Mungu aliahidi kupita juu yao.

¹¹⁰ Sasa, hiyo ni picha ya namna gani kwa ajili ya kanisa siku hizi! Sasa nitaharakisha, bali sina budi tu kulielezea hili hapa, kwa dakika moja tu. Siku hizi daima tunaliacha kusanyiko moja tukaingia lingine, tukihamisha makaratasi yetu kutoka kanisa moja, barua zetu, hadi lingine. Endapo Methodisti halifanyi jambo fulani unalowazia halipaswi kutendwa, utaipeleka kwa Baptisti; kutoka kwa Baptisti unaingia kwa Presbiteri; kutoka moja kuingia lingine. Mnaona? Kuna nini? Inaonyesha tu kwamba kamwe hujafikia mahali pale bado. Kamwe hujafikia mahali pale ambapo unaweza kutoa presha. Unaona? Unatazama kitu ambacho hupaswi kuwa ukikitazama. Wakristo, kutoka dhehebu moja hadi lingine, inaonyesha kwamba kamwe hawajapata kuja kwenye kimbilio hilo. Mnaona?

¹¹¹ Wanaenda wakati mwingine kwenye seminari. Hilo ni sawa. Nao wanajifunza Neno vizuri tu wawezavyo. Wanakuja nyumbani, na kujaribu kuzungumza Neno hilo vizuri kadiri tu dhehebu lao linavyowaruhusu kulizungumzia. Na hilo ni zuri. Bali hilo silo. Sio kulijua Neno Lake, bali ni kumjua Yeye. Yeye! Mbona, hakika! Sio kiasi cha Neno ukijuacho, jinsi ulivyo na kanisa zuri, yale dhehebu letu linayomaanisha kwa ulimwengu, ni maachilio mangapi tuliyo nayo kwa *hili*, na ni ushirika kiasi gani tulio nao pamoja na ulimwengu, ni umati wa namna gani unaokuja. Ni wewe. Je, uko chini ya damu? Endapo wewe, kama mtu binafsi, sijali kama kila mmoja wa kusanyiko amekosea, wewe ungali salama. Uko chini ya Damu.

¹¹² Wakati mwingine Mungu alikuweka kwenye kusanyiko baya, upate kumulika Nuru. Usirukeruke, kuendelea tu kuruka kutoka mahali pamoja hadi pengine, kutoka kitu kimoja hadi kingine. Dumu tu chini ya Damu. Ukianza kukimbia nje, basi usalama wako umekwisha. Kaa chini ya Damu.

¹¹³ “Jina ni ngome imara. Wenye haki huikimbilia, nao ni salama.” Toa presha. Mtazameni katika saa ambazo tunajua ya kwamba wapo watu walio chini ya Damu. Tunaliona likithibitishwa. Tunamwona Mungu, yale anayofanya kulithibitisha Kanisa Lake.

¹¹⁴ Tuliahidiwa kitu chochote tunapokuwa katika Ngome hii. “Lolote mwombalo katika Jina Langu, nitalifanya. Mkikaa ndani Yangu, na Maneno Yangu ndani yenu, ombeni mtakalo, mtatendewa.” Ni mahali pa jinsi gani! Imeandikwa, “Fanyeni mambo yote, lolote mfanyalo, lifanyeni katika Jina Langu,” sio mlifanye katika jina la kanisa.

¹¹⁵ Unasema, “Vema, ninatoa ushuhuda kwa sababu ninashukuru usiku wa leo mimi ni Mpresbiteri. Ninashukuru mimi ni Mpentekoste. Ninashukuru mimi. . .”

116 Ninashukuru mimi ni wa Kristo. Mnaona? “Jina la Bwana ni ngome imara.” Mnaona? “Wenye haki wanaikimbilia wakawa salama.” Basi, katika Jina Lake tunao ushirika.

117 Sasa, kama tukitoka hapa nje, na mmoja aseme, “Mimi ni mfuasi wa church of God.” Ninaamini hili ni church of God. Naye huyo mwingine aseme, “Mimi ni wa Assemblies,” vema, hiyo huenda likasababisha msugvano. Mmoja anasema, “Mimi ni wa United.” Huyo mwingine anasema, “Mimi ni mfuasi wa kitu kingine, Waumoja,” ama lolote lile. Kama mtazozana jinsi hiyo, mtazozana.

118 Lakini ikiwa kweli umefika kwenye Ngome ile, haijalishi uko na kikundi kipi, uko chini ya Damu. Basi hapo ndipo mahali pekee unapoweza kuwa na ushirika, wakati Damu ya Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, ikitusafisha na dhambi zote. Tunao ushirika basi, mmoja kwa mwingine. Ni ushirika wa jinsi gani! Tunaweza kufikia ng'ambo ya pili, na kulichukua church of God, Assemblies of God, Waumoja wa Mungu, na lolote liwezalo kuwa, haijalishi ni lipi. Hapo tuna mambo shirika. Tunaye Kristo, naye Kristo ndiye Kimbilio letu. Kila mmoja wetu, kama ni Mbaptisti, Mpresbieri, Mlutheri, Mkatoliki, chochote alichu, kama yupo chini ya hiyo Damu, unaweza kushiriki pamoja naye kwa kuwa ninyi ni mmoja. Mko katika ushirika huu wa Kiungu wa Kristo. Loo, ni jambo kuu jinsi gani!

Isaya alilielezea, “Yeye ni Mwamba katika nchi yenye uchovu.”

119 Hiyo ni nchi ya namna hii, ambako yeye anahofu sana, watu hawajui la kufanya. Wao wanasema, “Vema, hii ni kweli? Hiyo ni kweli?” Kristo ni mkweli. “*Hii* ndiyo njia? *Ile* ndiyo njia?”

Yeye alisema, “Mimi ndimi Njia.”

“Ukweli ni upi, *huu* ama *ule*?”

Yesu alisema, “Mimi ndimi Kweli. Mimi ndimi Njia, Kweli, Uzima.” Mnaona?

120 Tumeacha kuhofia hilo. Njia hiyo hupandisha presha. Mnasema, “Methodisti ni ya kweli? Presbiteri ni ya kweli? Mama yangu alikuwa ni *hili*. Na nanii wangu...” Lakini Kristo alikuwa ndiye Bwana wako. Mnaona? Haidhuru ni nini, unapandisha presha, na hiyo inawafanya kuzozana. Mnaona? Kama unategemea tu shirika lako, hiyo inachochea mzozano. Unajaribu kulijenga dhehebu lako. Bali ukiwa ndani ya Kristo, unatoa tu presha. Amina. Kuna chakula tu kwa ajili yetu sote. Jamani!

121 Yakobo alichimba kisima, nao Wafilisti wakamtoroka. Ninaamini alikiita “ugomvi.” Ninalisahau hilo jina. Lilikuwa hilo? Kisha akachimba kingine, nao wakamfukuza kutoka kwake, ndipo akakiita hicho “kijicho,” ama kitu fulani. Halafu akachimba kisima kingine. Akasema, “Ipo nafasi kwa ajili yetu

sote. Sote na tuingie.” Kwa hiyo nafikiri inatupasa kukiendea kisima hicho cha tatu. Kwa hiyo katika . . .

¹²² Njia pekee tunayoweza kufanya hilo, ni chini ya Damu, ndipo Mmethodisti anaweza kuingia moja kwa moja humu ndani na kujisikia nyumbani kadiri Mpentekoste awezavyo. Naam, bwana. Mchungaji Mmethodisti, aliyejazwa na Roho Mtakatifu, angeweza kuchukua kila Mpentekoste nchini, moja kwa moja mle ndani, na awe nyumbani kabisa. Nasi tunaweza kuwa nyumbani mmoja kwa mwingine, sio kwa sababu, twasema, sasa, “Ninyi Wamethodisti wote, ninyi Wapentekoste wote.” Mnapeosema, “Ninyi nyote Wakristo.” Amina! Loo, hilo linajumuisha kile kitu kikubwa. Ndipo tunakuwa na ushirika, na kutoa tu presha. Ninapenda hilo. Hakuna presha inayopandishwa basi. Hatujali wewe ni mfuasi wa nini, chapa unayovaa.

¹²³ Nilikuwa nikiwachunga ng’ombe. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . . Bonde la Mto Troublesome. Na ndipo kama unaweza kuchangia tani mbili za nyasi kavu, na kwenye ranchi hii, mbona, ungeweza kumweka ng’ombe kwenye hayo malisho. Na baadhi ya hao watu wana ng’ombe elfu moja, mbili. Grimes alikuwa huko juu, nguzo, Nguzo ya Almasi, yetu ilikuwa ni maskini Turkey Track. Mbona, wao, wao walikuwa na chapa nyingi, labda chapa ishirini ama thelathini, huku na huku katika hilo, ambazo shirika hilo lilikuwa nazo humo. Halafu, kulikuwako na uzio unaohama unaowazuia ng’ombe wasiingie kwenye msitu wa taifa, unapopanda kwenye magenge, na kuwaweka mle.

¹²⁴ Ndipo basi wapanda farasi wanaendesha kote kwenye kiangazi na kuwaweka dume kadhaa, ng’ombe kadhaa wa kike, na kadhalika. Ndipo sisi. . . Wanao uzio unaohama, naye mpanda farasi anasimama pale kuwakagua hao ng’ombe wanapoingia. Wakati mwingine kundi letu zima lingekutana wakati tukiwaleta hao ng’ombe huko, katika majira ya kuchipua majani. Nako kuna maelfu ya ng’ombe hasa huku na huku kwenye bonde hilo. Basi ni mara ngapi nimeketi kule huku mguu wangu umefunganishwa nchani mwa matandiko, nikimwalia mpanda farasi huyo amesimama pale. Yeye anawakagua hao ng’ombe wanapopita.

¹²⁵ Sasa, niliona kulikuwako na yapata . . . chapa za namna mbalimbali zilingia mle ndani, lakini huyo mpanda farasi kamwe hakutazama ile chapa. Yeye alitazama kwa makini kile kibandiko cha damu, maana hakuna kitu kinachoweza kuja kwenye msitu huo ila ukoo safi wa Hereford. Kwa hiyo, hiyo inadumisha haki zako za kuzalisha. Mnaona?

¹²⁶ Nafikiri hivyo ndivyo itakavyokuwa kwenye ile Siku ya Hukumu. Mungu hatasema, “Je, wewe ulikuwa ni mfuasi wa Assemblies, church of God?” Yeye ataangalia kibandiko hicho

cha Damu. “Nitakapoiona hiyo Damu, nitapita juu yenu.” Pasipo kujali chapa tuliyo nayo, hiyo haimaanishi kitu.

¹²⁷ Hivi wewe ni Hereford? Umesajiliwa? Je, wewe ni Mkristo aliyezaliwa mara ya pili, ukajazwa na Roho Mtakatifu, ukaoshwa katika Damu Yake? Hilo ndilo Mungu atakalotazamia, Siku ile, kukiona kibandiko hicho cha Damu. “Nitakapoona... Sio nitakapoiona chapa. Nitakapokiona kile kibandiko cha Damu, unaweza kupita uingie.” Amina.

¹²⁸ Ninaanza kujisikia kubarikiwa. Hapa ni karibu saa sita na nusu, nami nilipaswa kuwa nimemaliza dakika ishirini zilizopita, na ndipo ninapoanza kuhisi kubarikiwa vizuri sana. Loo, Mungu asifiwe! “Nitakapoiona ile Damu, nitapita juu yenu.”

Sasa, kwa dakika nyingine moja ama mbili, mkipenda.

¹²⁹ Ninaambiwa kwamba kuna aina fulani ya tai. Wengi wenu watu wa kanda mna ujumbe wangu juu ya *Tai Ataharikishavyo Kiota Chake*. Nami nilikuwa nikiwasoma tai. Nawapenda tai. Najua wanafikiri yeye ni maskini mhuni, lakini alikuwa hapa kwa kusudi fulani. Kama vile ni... nilimwambia mke wangu, hivi majuzi...

¹³⁰ Ndipo, nyote mmeona, katika gazeti la *Life*, ambapo waliwaua hao mbwa mwitu elfu mia nne na kitu mwaka jana, wakiwachukua tu na kuwapiga risasi. Wana kundi la nguruwe waliofugwa waliokurupuka kule chini. Watachukua tu, wataingia mle ndani kwa ndege, na kuwauwa kwa bombomu. Hayo ni mauaji ya kinyama. Hilo si sawa. Si haki. Mbwa mwitu huyo hawezi kujiepusha kuwa mbwa mwitu. Hana budi kuua, apate kula.

¹³¹ Mara nyingi wao wanasema anawaua wana-kondoo na kadhalika, namna hiyo. Iwapo kundi hilo la wafugaji wazembe walio nao kule juu... Wakati hao kondoo jike wanapojifungua, kama wangeenda huko nje na kuwashughulikia kondoo hao jike, badala ya kulala mpaka saa nne ama saa tano, mbwa mwitu angekuwa na jina bora zaidi. Hiyo ni kweli. Yeye si Don El, ki—kinyago usoni mwake. Yeye ni mbwa mwitu. Hakika. Nimewaona wanadamu walio wabaya kuliko yeye. Lakini...

¹³² Pia dubu, sikuzote wanazungumza kuhusu dubu, “Yeye ni mwuaji. Anawaua ndama.” Nimewinda tangu nilipokuwa mvulana mdogo, na kamwe sijawahi kumwona dubu akimwua ndama. Hakika, angeweza kumwua, wakati akifa kwa njaa. Wewe ungefanya vivyo hivyo.

¹³³ Kumbuka, huna budi kuua, upate kula. Na kila siku, leo hii, kama ukiishi, kitu fulani hakina budi kufa upate kuishi. Ukimwua ng’ombe; alikufa. Ukimwua kondoo; alikufa. Wasema, “Sili nyama.” Vema, kitu fulani kilikufa, kwa vyovyote vile. Ukila kiazia, kilikufa. Ni uhai. Ukila mboga za majani,

zilikufa. Ni uhai. Naye mwanadamu anaweza tu kuishi kwa vitu vilivyokufa.

¹³⁴ Sasa, lipateni. Basi kama ilibidi kitu fulani kife, kusudi upate kuishi kimwili, si ni wazi kwamba ilibidi kitu Fulani kife kusudi uweze kuishi kiroho? Kristo alikufa, sio kanuni ya imani, bali maisha yatokayo kwa Kristo. Tunaishi Milele, kupitia Kristo.

¹³⁵ Tai huyu, ni ndege mkubwa. Mimi si...sina wakati wa kulifafanua, yale afanyayo, na jinsi anavyokitengeneza kiota chake, na ambapo yeye si kama ndugu yake wa kimadhehebu, kuku, mkwaruza kibanda. Yeye atahakikisha hakuna kitakachowasumbua watoto wake. Anapanda juu sana. Hakuna kicheche atakayempata ama vifaranga wake.

¹³⁶ Aa, si ajabu Mungu alifananisha urithi Wake na tai! Mnajua, Yeye anajiita Mwenyewe tai. Nasi ni vifaranga wa tai. Naye tai si mla mizoga. Yeye hupata nyama mpya kila siku. Amina. Chakula cha tai, hicho ndicho Kanisa linachopaswa kuwa nacho, sio juu ya ujuzi wa miaka arobaini iliyopita. Ujuzi nilio nao sasa hivi, kitu kipya kutoka Mbinguni.

¹³⁷ Maskini tai wa kale hujenga kiota chake huko juu sana kwenye majabali, kusudi vicheche na kadhalika wasimpate. Ndugu yake wa kimadhehebu, kuku, huweka chake kwenye ufa wowote wa kale huko chini uani, anakwaruza bandani, na kila kitu kingine. Lakini si tai, asingeweza kula hicho. Mnaona? Ameondoka. Hicho si kitu kwake.

¹³⁸ Tai huyu, anapofikia mahali fulani, Biblia ilisema, “Kufanya upya ujana wetu kama tai.” Mara nyingi nilishangaa, “kufanya upya ujana,” hilo lingewezekanaje?

¹³⁹ Ninakumbuka. Hili linasikika...Nimechukua muda wenu mwingi sana. Bali, kundi la kwanza la kipentekoste nililopata kuwa pamoja nalo, yalikuwa ni madhehebu mawili ya hayo, pamoja. Nami nilikuwa nikishuka kutoka—kutoka kwenye ziara ya kuvua samaki, nami nikaingia. Nikaona majina haya kote juu ya hili. Nikaingia. Nikasikia kelele mbaya mno, nao watu hawa mle ndani, wakirukaruka, na kukimbia, na kucheza, kote mahali hapo. Nikawazia, “Kwani hii ni nini?”

¹⁴⁰ Kwa hiyo yeye akasema, “Wahudumu wote jukwaani usiku wa leo.” Na kulikuwa na yapata mia tatu wetu, basi tukapanda juu. Nikapanda na kuketi chini. Kasema, “Sasa, hatuna wakati kwa ajili yenu nyote kuhubiri.” Kasema, “Tunataka utaje tu jina lako, mahali unapotoka.”

¹⁴¹ Nilipofikiwa, nilisema, “William Branham, mwinjilisti; Jeffersonville, Indiana,” nikaketi chini.

¹⁴² Kwa hiyo nilikuwa nimewasikia baadhi ya wahubiri wazuri siku hiyo. Na muda si muda mwajua...Iliwabidi kuufanyia Kaskazini, kusudi watu weusi waweze kuhudhuria. Ulikuwa ni

mkutano wa kitaifa, nao iliwalazimu kuufanyia Kaskazini, siku hizo. Hiyo imekuwa kama miaka ishirini na mitano iliyopita, nadhani, ama zaidi, iliwabidi kuufanyia huko juu kusudi watu weusi waweze kuihudhuria.

¹⁴³ Kwa hiyo usiku huo nikawaza, “Jamani, mkutano huu mkubwa, mkutano huu wa usiku, watakuwa na mmoja wa wahubiri wao walio maarufu sana kuja.” Hakika, sisi Wabaptisti, mwajua, hivyo ndivyo tulivyolifanya. Kwa hiyo wakaninii. . .

¹⁴⁴ Baada ya kitambo kidogo, akiinuka pembeni, alikuwa ni mzee mweusi, mzee mweusi, alikuwa na mzingo mdogo wa sufi—sufi nyeupe kuizunguka shingo yake. Nami nilikuwa na yapata, nadhani, yapata umri wa miaka ishirini na miwili, ishirini na mitatu. Nao walikuwa wamevaa haya makoti ya kale ya wahubiri, moja ya haya ya mtindo wa kale yaliyokatawa nchani, mwajua, nyuma upande wa nyuma, mwajua, kama kijumbamshale. Naye maskini jamaa huyo mzee akaja akiyumbayumba namna *hii*, yapata umri wa miaka themanini. Akatoka nje kuninii. . . Nikawazia, “Mbona wamlete mtu kama huyo huku, kwenye mkutano hapa, ambapo yapata watu elfu moja mia tano wameketi hapa, na, hapo, mmoja wa wahubiri wao kujitokeza namna hiyo?”

¹⁴⁵ Maskini jamaa huyo mzee akajitokeza. Akasema, “Vema,” anasema, “nitawaambia.” Anasema, “Ninataka kuchukua somo langu kutoka Ayubu, usiku wa leo. ‘Ulikuwa wapi nilipoiweka misingi ya ulimwengu, hapo nyota za asubuhi zilipoimba pamoja na wana wa Mungu wakapiga kelele za shangwe?’”

¹⁴⁶ Niliwasikiliza wahudumu hao wote siku hiyo, jinsi ambavyo walikuwa wameuweka uhai wa Kristo katika Maandiko, vizuri sana. Nilidhani wahubiri halisi walikuwa wamezungumza siku hiyo. Nikawaza, “Maskini jamaa huyu mzee aliyelemaa.”

¹⁴⁷ Vema, kamwe hakuzungumza kuhusu yale yaliyokuwa yakitendeka duniani. Alizungumza juu ya yale yaliyoendelea Mbinguni. Naye akamchukua huko ng’ambo yapata miaka milioni kumi kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, akamshusha kupitia kwenye upinde mlalo wa mvua, na kule Kuja mara ya pili. Haikutimia kama dakika mbili akifanya hivyo. Ndipo alipofanya hivyo, Roho akamgusa. Akaruka juu hewani, akavigonganisha visigino vyake pamoja, kasema, “Utukufu kwa Mungu!” Akasema, “Hamna nafasi ya kutosha chumbani humu kwangu kuhubiri,” akatoka jukwaani kwa mwendo wa shoti.

¹⁴⁸ Nikawazia, “Hilo ndilo ninalotaka. Kama hilo litamfanya mzee kutenda jinsi hiyo, lingenitendea nini mimi?” Kufanya upya ujana wake! Mbona, alikuwa na nafasi kubwa zaidi kuliko tuliyo nayo hapa juu, kwaya na wote, na hata hivyo hawakuwa

na nafasi ya kutosha kumshikilia wakati Roho alipomgusa. Nikasema, “Hilo ndilo ninalotaka. Hilo ndilo ninalotaka.”

¹⁴⁹ Tai huyu mzee, anapata gamba usoni na kichwani mwake anapokuwa mzee. Ni vigumu kwake kula. Anakonda sana; mdomo wake hautafunguka vizuri. Karibu anaingia upofu. Nalo hilo gamba linapofikia mahali fulani kichwani mwake, wanasema yeye huruka juu sana hewani, na kukaa kule, naye anakigongesha kichwa chake mwambani, akilitoa gamba hilo, kama anaweza. Ndipo anayageuza macho yake na kuangalia nyuma. Analigongesha hilo gamba. Loo, halina budi kutoka. Lazima litoke. Lisipotoka, yeye atakufa. Hana budi kuondoa gamba hilo usoni mwake na mdomoni mwake. Naye angekigongesha kichwa chake kwa njia moja, kisha kwa njia nyingine. Anakigongesha mpaka analiondoa gamba hilo. Ndipo anapokigongesha kwenye mwamba huo mpaka hilo gamba linatoka, ndipo anapiga makelele, na kurusha mabawa yake mbele na nyuma, na kushangilia kwa sababu anajua atapata manyoya mapya; atakula vitamini zake tena; ataufanya upya ujana wake. Nikawazia, “Hilo ni jambo zuri jinsi gani kwa huyo tai. Hilo ni zuri.”

¹⁵⁰ Ila najua Mwamba ambao mwanadamu anaweza kuukaribia, naye anaweza kujigongesha, na kujigongesha, mpaka mashaka yote yamekwisha, mpaka wasiwasi na masumbuko ya ulimwengu yamekwisha. Ndipo akiisha kuligongesha gamba la dhambi likamwondokea, mpaka ile Damu imeitakasa nafsi yake, ndipo Uzima wa Milele hauna budi kuja. Anaweza tu kuketi kitako na kutoa presha, kwa sababu Uzima wa Milele ni hakika.

¹⁵¹ Loo, enyi tai, leo hii, hiyo ndiyo sababu mpo hapa. Ninyi ni watoto wa tai. Lakini kama gamba limeanza kuyapofusha macho yenu, masumbuko ya ulimwengu, ama hamwezi tu kumeza Chakula chote cha Mungu, hebu tuje kwenye Mwamba huo katika nchi yenye uchovu. Hebu tuje Hapo na kujigongesha madhabahuni mpaka gamba limevunjika, na macho yetu yanaweza kumwona dhahiri, Yesu tena, na masumbuko ya ulimwengu huu yamepita. Ndipo presha itaondoka. “Yeye ni Mwamba katika nchi yenye uchovu, Kimbilio katika wakati wa dhoruba,” Kimbilio, Mahali pa raha, kwa ajili ya waliochoka. Hebu tuje Mahali hapa.

Na tuinamishe vichwa vyetu kwa dakika moja.

¹⁵² Samahani kwa kuwaweka muda mrefu. Kulikuwa na kama vipande sita vya muhtasari huu vilivyowekwa hapa, mawazo madogo na Maandiko niliyokuwa nikitaka kuyatumia. Lakini wakati umekwisha. Loo, ewe mtoto wa tai, labda maskini msichana mdogo, mvulana mdogo, ama labda mzee fulani, ama mtu wa makamu, kwa nini upo hapa asubuhi ya leo? Kwa sababu kwamba, wewe, wewe kweli ni tai. Lakini labda masumbuko ya

maisha haya kidogo yamekupiga vita kote, vibaya. Umekuwa kipofu. Huna uhakika sana tena, mahali unapokanyaga kwa mguu wako. Hebu na tuukaribie tu ule Mwamba sasa. “Loo, niongoze kwenye Mwamba ule ulio juu kuliko mimi.” Jalia nikae kwenye Mwamba huu. “Yeye ni Ngome wakati wa dhoruba.”

¹⁵³ Anza kujigongesha mlangoni sasa hivi, kujigongesha kwenye mlango wa Mwamba huu. Yeye atafungua. Gamba litaruka liondoke. Ndipo presha itakuacha, nawe unaweza kuwa na raha tena, presha yote imeondoka. Unaweza kuja kanisani. Haijalishi mchungaji anahubiri juu ya nini. Mradi tu anadumu kwenye Neno hilo la Mungu, kamwe halitakuhukumu. Tayari umejitia nanga Humo. Uko sawa kabisa sasa.

Na tuombe.

¹⁵⁴ Bwana Yesu, ninataka kuelezea tena, Bwana, katika kutoa shukrani kwamba kuna mahali padogo hapa Phoenix, na kote mahali mbalimbali. Na hapa ni mojawapo ambapo, mimi—mimi mwenyewe, na—naweza kuja na ninaweza kuona raha. Hakuna kitu kinachonifunga mimi. Ni—ninayasema tu haya Maneno. Hapo ni mahali pa jinsi gani; huru, presha yote imeondoka. Nina shukrani sana kwa ajili yake, Bwana.

¹⁵⁵ Ee Bwana, jalia Mwamba ule mkubwa daima ukae kwenye madhabahu haya, ambapo maskini watoto wakaidi wa tai, kote mjini, wanaweza kuingia na kutambulishwa mahali fulani, watakapoligongesha gamba la ulimwengu liwaondokee, ambapo wanaweza kufurahia ushirika huu, kwa kutoa presha, katika siku hizi za wakati wa atomiki ambapo ulimwengu umetishika. Kila taifa linatetemeka. Mbingu zinatikisika. Maumbile yote yanalia. Ulimwengu wenyewe unatetemeka kwa kuwa unaweza kulipuliwa vipande-vipande. Lakini tunao Ufalme usioweza kutikisika. Tunao Mji wa kimbilio. Tuna Gosheni, ambako jua halitashuka kamwe. Tujalie, Bwana. Jalia tuje kwenye Mwamba huu sasa.

¹⁵⁶ Kama sungura mdogo, hadithi yake, mbwa wawindaji walikuwa nyuma yake. Angeweza kuhisi pumzi yao yenye joto juu ya miguu yake. Muda kidogo tu, mruko mwingine mmoja ama miwili, na huyo mbwa angemshika maskini jamaa huyo. Angemewa kwa pupa, katika muda mfupi tu. Lakini baada ya muda kidogo akaona shimo mwambani. Ndipo akawazia, “Laiti ningaliweza tu kufikia mwamba ule, ndipo niko salama.” Mara yule mbwa alipofanya mruko wa mwisho kwake, alihisi pumzi yake yenye joto kwenye visigino vyake, lakini akakimbia chini ya ule mwamba. Ndipo angeweza kuketi chini na kutoa presha. Huyu mbwa asingeweza kukwaruza kupitia kwenye mwamba huo.

¹⁵⁷ Bwana Yesu, ninakuomba Wewe asubuhi ya leo, Bwana, kwamba kama baadhi ya maskini viumbe hawa Wako, ambao wamezurura kutoka eneo lile la usalama; wanaweza kuhisi pu—

pumzi ya mbwa wa kuzimuni, wasichana, vijana wanaume, wakienda mbio nyuma yao, wakiona maisha yao yakiharibika upande ule mwingine. Jalia waharakishe asubuhi ya leo kwenye ufa huu kwenye Mwamba. Kunao mmoja. Wenye haki huukimbilia, wakawa salama. Tujalie, Baba, kupitia kwa Yesu, Mwana Wako.

¹⁵⁸ Wakati tumeviinamisha vichwa vyetu, na mioyo yenu imeinamishwa, pia, ungeweza, kama huko katika Mwamba huo asubuhi ya leo, waweza kuinua mkono wako kwa Mungu? Na kusema, “Mungu, jalia niingie kwenye eneo hilo la salama sasa, kwamba ambamo ninaweza tu kutoa presha. Kidogo nimekuwa mchovu. Nimeanza kuona nikichukuliwa na mkondo. Nilijisikia nikiondoka. Sina ujuzi niliozoea kuwa nao. Nirudishe kwenye ule Mwamba upesi sana, Bwana.” Ungeweza tu kuinua mkono wako, useme “Niombee, Ndugu Branham”? Mungu awabariki. Hilo ni zuri, kote kila mahali. Ah, hilo ni jema. Mungu awabariki.

¹⁵⁹ “Nirudishe kwenye huo Mwamba, Bwana. Nirudishe. Ninachukuliwa na mkondo. Loo, usiniache niondoshwe kwake. Nijalie. . . Kama nitakula, jalia nile karibu na ule ufa. Jalia nikae karibu na mahali Mana inapoangukia. Hainibidi kutangatanga nje. Mana imewekwa papo hapo mlangoni.”

¹⁶⁰ Baba wa Mbinguni, Wewe uliona kundi hili la mikono. Ninaomba ya kwamba utawapa shauku zao. Jalia gamba lote ambalo limeanza kuwapofusha sasa, Bwana, wakati mioyo yao ikidundadunda, na moyo wao wa kiroho ukidundadunda, yaondolee mbali mashaka yote, kutokuamini kwote, kuchanganyikiwa kwote, wasiwasi wote, na—na kushangaa ni kitu gani *hiki* ama *kile*, wasiwasi wote. Jalia sasa hivi kwa utamu waone kwamba gamba linavunjwa, wakati wakigongesha kwa nguvu sana maombi yao kwenye ule Mwamba. Jalia Kristo awalete juu sasa na kuwaweka juu ya mnara mrefu. Nao wanaweza kupigapiga maskini mabawa yao ya kiroho, waseme, “Niko huru. Niko huru.” Tujalie hilo, Baba, katika Jina la Yesu.

¹⁶¹ Na sasa kuna wale hapa asubuhi ya leo walio kwenye hilo kimbilio, nawe ni mgonjwa, wala hujui kile kitakachotokea, nawe unataka kutiwa nanga katika kitu kitakachokupa usalama, kitakachouponya mwili wako, nawe unataka kukumbukwa katika maombi?

¹⁶² Kumbukeni tu, maombi mafupi tu; hivyo tu. Shindilia nguzo ndogo hapo mahali umeketi, huku ukisema, “Leo hii, leo hii, maombi ya imani yaliombwa kwa ajili yangu. Na kila wakati ninapoingia kwenye kanisa hili, nitakumbuka ambapo nilikuwa nimeketi asubuhi ya leo. Hapo maombi ya imani yaliombwa na kusanyiko zima, kwa ajili yangu. Nitapata afya sasa. Ndilo hili. Ninalitatua.” Sasa, inua mkono wako, ukisema, “Ninashindilia nguzo yangu chini, sasa hivi.” Mungu akubariki.

¹⁶³ Sasa, kumbukeni, kwa imani, shindilia nguzo chini, sasa hivi, papo hapo ulipoketi. Leo hii, Jumapili, tarehe kumi, ninaamini ndivyo ilivyo, ama tarehe 13. “Siku hii ya 13 ya Januari, katika kanisa hili dogo la Mungu, penye kiti fulani hiki, ninaomba maombi ya imani, pamoja na mhudumu, na pamoja na mwinjilisti, na pamoja na kusanyiko; mmoja akimwombea mwenziwe. Hii ndiyo siku ya uponyaji wangu, papa hapa. Ninalitatua, papa hapa, Bwana. Mimi ni tai Wako. Niko kwenye eneo la kimbilio. Ninayo haki ya kila baraka ya ukombozi ambayo Yeye alininunulia. Mimi hapa, papa hapa sasa.”

¹⁶⁴ Baba wa Mbinguni, ninawaleta Kwako. Ninayaweka maombi yangu pamoja na yao. Na sasa, kwa imani tunainuka kutoka kwenye kanisa hili, na kuendelea huko juu ya yale maeneo, na angahewa, na maeneo, na maeneo, kuendelea kupita nyota, mwezi, kupita lile Kundi Jeupe la Nyota kwenda juu, hadi kwenye kiti cha enzi cha Mungu Baba yetu, ule upinde mkubwa wa mvua unaokingama madhabahu yale ya pembe za ndovu. Hapo kwenye madhabahu hayo pamewekwa Dhabihu inayotokwa na damu. Nasi tunaangalia mgongoni Mwake, kama vile nabii alivyotuagiza kufanya, na kusema, “Kwa mapigo Yake sisi tuliponywa.” Baba, ninamleta kila mmoja wao Kwako. Na Yeye alisema, Mwenyewe, “Mkimwomba Baba lolote katika Jina Langu, nitalifanya.”

¹⁶⁵ Sasa, Baba Mungu, ninawaombea watu hawa wagonjwa. Wameshindilia nguzo chini, asubuhi ya leo. Ninaliamini kwa moyo wangu wote. Hii ndiyo saa ya maombi ya imani. Nami ninaamini, wakati nikikuomba Wewe kumponya kila mmoja wao. Wanakubali. Nasi hapa tunashindilia nguzo, kama kumbukumbu kwamba tulikuwa kwenye kiti cha enzi cha Mungu asubuhi ya leo. Limetatuliwa. Mungu alifanya ahadi.

¹⁶⁶ Sasa, Bwana, imeandikwa katika Marko Mtakatifu, mlango wa 11 na kifungu cha 22, cha 23, “Ukiuambia mlima huu, ‘Ng’oka,’ usitie shaka moyoni mwako, bali uamini kwamba yale uliyosema yatatimia, yale uliyosema yatakuwa yako.” Bwana, limesemwa, sasa na litimie. Katika Jina la Bwana Yesu Kristo, ninalikubali kwa ajili ya kila mmoja, na kwa ajili ya utukufu Wako.

¹⁶⁷ Sasa, amini kwa moyo wako wote. Na huku vichwa vyetu vimeinamishwa, hebu tuimbe wimbo huu wa kale wa kanisa, *Nampenda*. “Nampenda kwani alinipenda kwanza, na kununua wokovu wangu mtini Kalvari.” Hivi unakubali kwamba uponyaji wako, wokovu wako, roho yako iliyofanywa upya, ikija katika nyumba ya kimbilio? Unalikubali? Inua mkono wako, useme, “Ninalikubali. Ninaliamini. Sasa hivi ninaliamini.” Vema, sote pamoja sasa.

Nampenda,

Na tumwabudu Yeye sasa.

Napenda...

Asante, Bwana, kwa kutoa magamba kutoka machoni mwangu.

Kwani, alipenda kwanza...

Ubaridi wangu wote umefifia sasa. Maradhi yangu yameondoka.

Kununua wokovu wangu
Pale Kalvari.

¹⁶⁸ Sasa, wakati tukiuiimba huo tena, ninawatakeni tu ku—kuushika mkono wa mtu fulani, mbele yako, nyuma yako, kando yako. Useme, “Mungu akubariki, msafiri, ndugu, dada. Nina furaha kufanya ushirika huu pamoja nawe.” Endeleeeni kuniombea mnapofanya jambo hilo sasa, tunapoiimba tena sasa.

Na...
Kwani alinipenda kwanza;
Na kununua woko-...

¹⁶⁹ Kabla sijaigeuza ibada kwa mchungaji, hebu na tuinue tu mikono yetu sasa, na kwa moyo wetu wote tuimbe huo kwa kilindi cha nafsi zetu. Mnampenda? Semeni, “Amina.” [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Hebu tuseme tena, “Amina.” [“Amina.”] Hilo linamaanisha “Na iwe hivyo.” Nampenda. Sote pamoja sasa, hebu tuuimbe, kwa sauti zetu zote.

Na...na...

¹⁷⁰ Mchungaji. Mungu awabariki. Samahani kwa kuwaweka muda mrefu, hata hivyo. [Mchungaji anasema, “Ni sawa.”—Mh.] Asante. 

63-0113M Kutoa Presha
Church Of God
Phoenix, Arizona Marekani

SWAHILI

©2020 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org